

Kunguru Koria alitamani kuwa mrembo. Aliwaonea wivu Kasuku na Tausi wenye rangi nzuri.

Kunguru Koria pia alivutiwa na rangi za mkia wa Tausi. Kila alipowaona Tausi na Kasuku aliwaangalia bila kuwamaliza kutokana na urembo wao.



Siku moja kunguru Koria alikuwa anatafuta chakula. Alivutiwa na harufu nzuri ya chakula. Aliifuata harufu ilipokuwa inatokea.

Alipofika aliona watu wa rika mbalimbali walikuwa wakisherehekea. Wengine walikuwa wakila na wengine wakicheza ngoma kwa furaha.



Kunguru Koria alivutiwa na sherehe ile. Japokuwa alitamani sana chakula, alivutiwa na msichana aliyevalia kitenge chenye rangi za kupendeza na yule aliyevalia hereni.

“Ooh, ona hereni za yule msichana, ni nzuri sana zinamfanya avutie,” alijisemea Kunguru Koria.

Kila alipocheza hereni zake nazo zilichezacheza na kutoa mlio mzuri.
Kunguru Koria alitaka kuwa na hereni, alitaka kuzivaa.

Alimwangalia yule msichana, alitamani zile hereni zidondoke ili aziokote aruke nazo.





Kunguru Koria alitulia juu ya tawi la mti. Moyoni aliazimia kuwa mrembo wa kuvutia zaidi ya Kasuku na Tausi. Watu walipomuona Kunguru Koria walimfukuza, walijua kuwa amekuja ili kudokoa chakula chao.

Kunguru Koria akaruka na
kuondoka kwa woga na unyonge.





Asubuhi alikwenda sokoni kwa muuza hereni, alimuuliza muuza duka kama anaweza kununua hereni.

“Utanilipaje? Wewe ni kunguru!” Alisema muuza hereni na kumfukuza Kunguru Koria.



Kunguru Koria aliwaza kisha alipata suluhisho.

“Nitakwenda kwa sonara. Ataweza kunisaidia, ninataka kuwa mrembo.”

Alijisemea Kunguru Koria kisha aliruka hadi kwa sonara. Alimkuta yuko kazini akitengeneza hereni.

“Nitakusanya makopo ya shaba na fedha kwenye majalala. Hivyo utaweza kutengeneza hereni nyingi nami utanipa jozi moja,” Kunguru Koria alimwambia sonara. Sonara alikubali.



Siku iliyofuata, Kunguru Koria kwa furaha alikwenda kutafuta makopo. Lakini hakukuwa na makopo kwenye mtaa wa kwanza. Aliruka hadi kwenye pipa la takataka la mgahawa uliokuwa mtaa wa nne. Alikusanya baadhi ya makopo kutoka kwenye pipa hilo.

Aliruka hadi kwenye nyumba za watu. Akiwa angani Kunguru Koria aliangalia chini kwa makini sana kutafuta makopo. Aliendelea kukusanya makopo ya fedha na shaba hadi alipoona kuwa ana mzigo wa kutosha. Akaruka na kuanza safari ya kuelekea kwa sonara.

Kwa kuwa alikuwa na kazi nzito ya kukusanya makopo, alihisi njaa. “Mh harufu nzuri hiyo, Nitashuka kopo lenye nyama hiyo, nitakula haraka, sitachelewa,” alisema Kunguru Koria.

Alianza kufuata harufu ile ya chakula iliyokuwa ikisambazwa na upepo. Alilitafuta hadi akalipata kopo lenye mabaki ya nyama. “Leo nitakula na kushiba chakula hiki kitamu,” alisema Kunguru Koria. Alitua mfuko na kuanza kula mabaki ya nyama yaliyokuwa kwenye kopo lile.
Aliposhiba aliruka na kuondoka kuelekea kwa sonara.






Wakati Kunguru Koria anafika kwa sonara hakuamini macho yake, “Loh! Sonara amekwisha ondoka?” Alijiuliza mwenyewe huku akitaharuki.

Alibaki amesimama akishangaa kufuli lililokuwa linaning’inia mlangoni. Furaha ya kuwa mrembo iliingia dosari. Alipoteza uchangamfu wote aliokuwa nao. Alitamani kulia.

Kasuku mrembo aliyekuwa kwenye mti wa karibu alitua pembeni ya Kunguru Koria. “Nini kimekupata Kunguru Koria?” Aliuliza Kasuku mrembo. “Nilikuwa na nafasi ya kuwa mrembo, kama ningewahi kufika, na kumkuta sonara.

Chakula nilichokula njiani kimeniponza, tazama sasa nimechelewa na sonara amekwisha ondoka!” Alisema Kunguru Koria.






Siku iliyofuata, Kunguru Koria alifika kwa sonara asubuhi sana.
Alimsubiri sonara kwa shauku kubwa.

Sonara alipowasili alichukua mfuko aliokuwa nao Kunguru Koria bila kusema neno lolote. Alitengeneza hereni nzuri na kumpa Kunguru Koria.

Koria alifurahi sana.



Alimuomba sonara amsaidie kumvalisha hereni. Sonara yule akamwambia, “Inakubidi kwanza uende ukatoboe matundu kwenye masikio yako, kisha ndio uvae hereni.”

Kunguru koria aliondoka akiwa na furaha sana. Aliwaza kwenda kwa Kasuku na Tausi ili wamtoge masikio. Aliwaza jinsi atakavyopendeza.





“Hatuwezi kutoboa matundu kwenye masikio yako maana masikio yako ni madogo sana.” Tausi na Kasuku walimwambia Kunguru Koria. Hakuwaamini Tausi na Kasuku.

Koria alipaa na kuondoka kwa hasira kwenda kutafuta msaada wa kutoga masikio yakekwingine .

“Lazima nitoge masikio, ningekuwa na uwezo ningejitoga mwenyewe. Lazima nivae hereni nitakuwa mrembo tu!” Alisema Kunguru Koria akiwa anaruka kuelekea kijijini.



Alipofika kijijini, alikwenda kumtafuta msichana mmoja kati ya wale aliowaona kwenye sherehe. Alipomuona msichana mmoja alimsogelea akatua karibu yake akaanza kumsemesha,


**“Kroo! Kroo! Kroo!”**


Msichana yule hakumuelewa Kunguru Koria, hivyo alimfukuza.




Kila alipojaribu kwenda alifukuzwa. Sasa alikuwa amechoka na mwenye njaa, Kunguru Koria aliziweka hereni zake chini ziling’aa zaidi.
Kunguru Koria hakukata tamaa aliamini atapata tu njia ya kutoga masikio yake ili avae hereni.

“Mchana umeshafika ngoja nikatafute chakula kwenye makopo, nile, nishibe ndipo nitafute njia ya kutoga masikio yangu. Nami nitakuwa mrembo tu.” Kunguru Koria alisema, aliruka na kuondoka.





Mwanga wa jua ulizimulika hereni, ziling’aa zaidi.



Koria aliziangalia zinavyong’aa akiwa angani. Hapo hapo akagundua kuwa nae akimulikwa na jua anang’aa. “Manyoya yangu yanang’aa kwa upande wa kulia.”

Aliruka juu akajiangalia tena. “Manyoya yangu yanang’aa kwa upande wa kushoto bila hereni.” Alisema Kunguru Koria.

Kunguru Koria aliruka ruka na kushangilia kwa furaha huku akisema, “Sitaki tena hereni, manyoya yangu yanang’aa na kupendeza, ninapendeza bila ya hereni.”

Kunguru Koria alitabasamu, na aliamua kutafuta chakula kitamu.
“Kunguru Koria!” Sauti iliita alikuwa ni Tausi.
“Hizo ni hereni nzuri.”
“Asante sana, ila nimegundua hata manyoya yangu yanang’aa. Ninapendaza ninavyong’aa hata bila hereni.”

